



*Sauti ya*

**HALIUZWI**

# TUICO

TOLEO NA: 21

Aprili - Juni, 2018



## **TUICO NA MAADHIMISHO YA MEI MOSI**



TUICO NA MEI MOSI .....	2
ADHIMISHA MEI MOSI KWA KUJIUNGA NA TUICO .....	3
TUICO NA MAADHIMISHO YA MEI MOSI .....	5
DHANA YA AFYA NA USALAMA KAZINI .....	7
WAJIBU NA HAKI ZA VIONGOZI WA TUICO KWA MWAJIRI KATIKA UBORESHAJI WA UTENDAJI KAZI .....	12
MIKATABA YA AJIRA.....	14
UCHUMI WA VIWANDA KUZINGATIA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI .....	17
MGOGORO WA WAFANYAKAZI WA MUFINDI PAPER MILLS ....	18

*“Jenga Chama imara na imarisha mshikamano”*



### BODI YA UHARIRI

#### Mwenyekiti

Boniface Y. Nkakatisi

#### Mhariri Mkuu

Dotto Kuhenga

#### Wajumbe

Samwel Lyimo

Issa Sadallah

Tamim Salehe

Noel Nchimbi

John Shikunzi

Margaret Ndagile

Fredrick mng'ong'o

Silpha Kapinga

#### Msanifu Mkuu

Haji Iddi

hajiddi@gmail.com



Jarida la *Sauti ya* **TUICO** hutolewa na Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri.

#### Ilala Sharifu Shamba

S.L.P. 5680, Dar es Salaam

Simu: 2866910, 2866959/60

Fax: 2866911

E-mail: tuico2004@yahoo.com

## TUICO NA MEI MOSI

**S**herehe za Mei Mosi mwaka 2018 ziliratibiwa na Chama cha TUICO. Huu ni utaratibu tuliokubaliana ndani ya Shirikisho letu la TUCTA kwamba kila mwaka kipatikane Chama kimoja cha kuratibu na kuandaa Sherehe za Mei Mosi.

Ndugu Wanachama na Wafanyakazi wote kwa ujumla, napenda niwajulishe kuwa Sherehe ya Mei Mosi ni muhimu sana kwa Wafanyakazi wote. Chimbuko lake ni madai ya kupunguza saa za kufanya kazi kutoka saa 10 mpaka 16 kwa siku hadi saa 8 bila kuathiri kipato cha Mfanyakazi.

Waajiri hawakufurahia madai hayo hivyo ilibidi wafanyakazi waanzishe mapambano makali nchini Marekeni kushinikiza Waajiri kukubaliana na dai hilo. Maandamano na migomo iliendeshwa na wafanyakazi wengi walishiriki kikamilifu. Katika migomo na maandamano hayo Wafanyakazi wengi walipigwa na kuumizwa na wengine wengi walipoteza maisha.

Mwaka 1889 Mkutano wa pili wa Kimataifa wa Kisoshalist (2<sup>nd</sup> International Socialist Conference) uliofanyika Paris – Ufaransa ulitangaza rasmi kwamba Mei Mosi ni siku ya Wafanyakazi wote Duniani, itakayoadhimishwa na Wafanyakazi wote. Kuanzia wakati huo sikukuu hii ikawa inaadhimishwa na Wafanyakazi wote Duniani.

Hapa kwetu Tanzania Wafanyakazi pia huadhimisha siku hii kwa kufanya shughuli mbalimbali. Kwa mwaka 2018 Sherehe za Mei Mosi zilifanyika kitaifa mkoani Iringa na Wafanyakazi kutoka Vyama vyote shiriki vya TUCTA vilivyopo Mkoani Iringa vilishiriki kikamilifu katika maadhimisho hayo. TUICO kama Mratibu wa Mei Mosi 2018 ilifanya shughuli nyingi mwezi April kwa ajili ya kuadhimisha Mei Mosi. Chama kilitembelea Wanachama katika sehemu zao za kazi na kuendesha semina mbalimbali zikiwa na lengo la kuwaelimisha Wanachama na kuwahamasisha ili washiriki kikamilifu katika sherehe za Mei Mosi. Aidha Chama pia kiliandaa



Kongamano kubwa la Tanzania ya Viwanda na kuhudhuriwa na Wanachama na Viongozi kutoka Vyama vyote Shiriki vya TUCTA na Watendaji wa Serikali Mkoni Iringa.

Mei Mosi inatukumbusha kwamba hali ya Wafanyakazi ilivyo sasa duniani inatokana na mapambano yaliyoendeshwa na Wafanyakazi na Vyama vyao enzi hizo ya kudai HAKI na MASLAHI yao. Mapambano haya hayawezi kusahaulika na tutayaendeleza wakati wote.

Hapa Tanzania Wafanyakazi wote kwa ujumla wetu tunatakiwa tujiunge na Vyama vya Wafanyakazi vilivyopo ili kuwa na nguvu ya pamoja ya kudai Haki na Maslahi yetu. Hii inajumuisha kudai kipato kizuri, Mazingira mazuri ya kufanya kazi, Huduma bora za Kijamii mfano Tiba, Maji Safi, Chakula n.k.

Sisi kama TUICO tunawahimiza Wafanyakazi wote walio katika Sekta zetu (Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri) kujiunga na TUICO ili tuweze kuwa na nguvu ya Pamoja ya kukaa na Waajiri na kufanya majadiliano yatakayowezesha kufungwa kwa Mikataba ya Hali Bora ambayo itaboresha maslahi kwa Wafanyakazi katika maeneo yote.

Umoja wetu ndio nguvu yetu. Tujiunge na TUICO sasa. Wakati ni Huu.



# ADHIMISHA MEI MOSI KWA KUJIUNGA NA TUICO

***Na: Fredrick Mng'ong'o,  
TUICO.***

- Chimbuko la Mei Mosi
- Changamoto zinazowakabili Wafanyakazi
- Changamoto hizi zinaweza kutatuliwa kwa kupitia Vyama vya Wafanyakazi kama vile TUICO.

## 1: IJUE TUICO

**T**UICO ni Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO).

Ni Chama Huru cha Wafanyakazi ambacho lengo lake si kupata kipato au faida bali kutetea haki, heshima na Maslahi ya Wanachama wake na Wafanyakazi kwa ujumla.

Mchakato wa kuundwa kwa TUICO ulianza mwaka 1991. Sheria ya OTTU Na. 20 ya mwaka 1991 iliipa hadhi OTTU kusimamia Uundaji wa Vyama Huru vya Wafanyakazi. Kipindi cha Mpito kilianza Desemba, 1991 na kuendelea hadi mwaka 1995.

Na katika mchakato huu, Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha Huduma na Ushauri (TUICO) kilifanya uchaguzi wa viongozi wake kwa ngazi ya Taifa tarehe 12, Mei, 1995 Mjini Arusha na shughuli za Chama kuendelea kuendeshwa chini ya Usimamizi wa OTTU.

Mwaka 1995 OTTU ilibadilishwa na kuwa Tanzania Federation Free Trade Unions (TFTU). Ni kipindi cha TFTU ndipo TUICO Ilianza rasmi shughuli zake kama Chama



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu Mhe. Jenister Mhagama, Waziri wa Viwanda Mhe. Mwijage na Viongozi wengine wakiimba wimbo wa mshikamano katika kongamano la Tanzania ya Viwanda lililoandaliwa na TUICO Tarehe 27/04/2018 mjini Iringa.*

Huru cha Wafanyakazi tarehe 01 Januari, 1996.

## 2: MUUNDO WA CHAMA

Ili kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi Chama kina muundo ufuatao:-

Chama kimegawanyika katika Sekta nne ambazo ni:-

- Sekta ya Viwanda
- Sekta ya Biashara
- Sekta ya Taasisi za Fedha
- Sekta ya Huduma na Ushauri

Chama pia kina Idara, Vitengo na Kamati mbali mbali katika utekelezaji wa shughuli zake, Chama kinajiendesha kuanzia ngazi ya:-

- Matawi
- Mikoa
- Kanda
- Taifa

## 3: MADHUMUNI YA TUICO

Madhumuni ya Chama yamefafanuliwa kikamilifu katika Katiba ya TUICO Sura ya pili (2:1):-

- Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini.
- Kushirikiana na kujadiliana na Waajiri katika Kuunda Kamati za Majadiliano na kuanzishwa kwa Mabaraza ya Wafanyakazi ili kudumisha amani mahali pa kazi.
- Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya Mwajiri na Mwanachama au Mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya Amani kila itakapowezekana

kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Hali Bora za Kazi.

Aidha kushirikiana na wahusika wengine katika kusimamia utekelezaji wa TUZO, Kanuni za Utumishi na Sheria nyingine za Kazi zitumikazo nchini.

- Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na Vyama Vingine vya Wafanyakazi nchini pamoja na vile vya Kimataifa.
- Kuwasiliana na Serikali kuhusu haja ya kutunga Sheria sahihi za Kazi na kuandaa Sera za kuendeleza Uchumi na maisha ya jamii.
- Kulinda maslahi ya Wanachama kwa kusaidia Serikali kuepukana na Uandaaji wa Sera ambazo hazina manufaa kwa Wafanyakazi.

#### 4: MAJUKUMU YA CHAMA

- Kuhamasisha na kuingiza Wanachama, nguvu ya Chama ni wanachama wake. Hivyo Chama kina jukumu la kuhamasisha Wafanyakazi mahali pa kazi na kuwaingiza katika Chama.
- Kutoa elimu na Mafunzo – Elimu ni Msingi wa Maendeleo, kwa kutambua hilo Chama hutoa elimu na mafunzo kwa Wafanyakazi, Wanachama na Viongozi ili kuweza kuwajengea uwezo katika Nyanja mbali mbali kama Sheria za Kazi na Chama kwa ujumla.
- Kukusanya na kusimamia Mapato ya Chama ili kuendesha na kutekeleza kazi za Chama, nguvu ya pesa (Kiuchumi) ni muhimu. Hivyo

ni jukumu la Chama kukusanya na kusimamia Mapato ya Chama kutoka katika vyanzo mbali mbali kama michango ya wanachama ambacho ni chanzo kikuu cha mapato.

- Kujadili na kufunga Mikataba ya pamoja - Lengo kuu la Chama ni kudai, kutetea na kulinda haki, heshima na maslahi ya Wafanyakazi. Ili kutekeleza hili, Chama hujadili na kufunga Mikataba ya Hali Bora na Waajiri kwa manufaa ya Wafanyakazi.
- Kuunda Kamati mbali mbali za Chama – Chama **kuunda** Kamati mbali mbali ili kutekeleza kazi zake - Kamati hizi huundwa kulingana na mahitaji na muda husika. Kamati hizi ni pamoja na zile za Makundi Maalumu kama Wanawake, Vijana na Walemavu.
- Utetezi na Uwakilishi wa Wanachama – Chama pia kina jukumu la kutoa utetezi na uwakilishi wa Wanachama. Pale inapotokea Mfanyakazi au Wafanyakazi wanashauri, au Mgogoro Chama husimamia utetezi na uwakilishi ili Mfanyakazi aweze kupata haki na maslahi yake.
- Kufanya Mikutano na ziara sehemu za kazi – Chama hufanya ziara na Mikutano mahali pa kazi ili kubainishachangamoto z i n a z o w a k a b i l i wafanyakazi na kuzitafutia ufumbuji.

#### 5: MANUFAA YA KUJIUNGA NA TUICO

Kwa kuzingatia misingi na madhumuni ya TUICO, manufaa ya kujiunga na TUICO ni pamoja na:-

- Mwanachama kustawi kiuchumi (Prosperity)
- Mwanachama kuwa na usalama wa ajira na afya yake pamoja na familia yake (Security).
- Mwanachama kuwa sawa na wengine bila kujali tofauti za elimu na maumbile, kabila, dini n.k (Equality)
- Mwanachama kuwa na uwezo kukabiliana na maisha hata wakati wa mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia (Sustainability).
- Mwanachama kuendesha Chama katika misingi ya kidemokrasia na uwajibikaji (Democracy and Accountability).
- Mwanachama kuwa mbunifu katika kazi yake ili kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia (innovative).
- Mwanachama kuwa na uwezo wa kuchagua fursa za kimaendeleo zinazojijiri katika soko la ajira (choice).
- Kutetewa katika Migogoro ya kikazi

#### KUJIUNGA NA TUICO

Ili kujiunga na Chama, basi wasiliana na Ofisi za TUICO zilizopo katika kila Mkoa hapa nchini au Makao Makuu ya Chama:-

Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO),

Ilala Sharrifu Shamba,

S.L.P. 5680, **DAR ES SALAAM.**

Simu: 2866910, 2866959/60

Fax: 2866911

E-Mail: tuico2004@yahoo.com

**“Jenga Chama Imara na Imarisha Mshikamano”**

# TUICO NA MAADHIMISHO YA MEI MOSI

**Na: Samwel Lyimo,  
TUICO.**

## 1. UTANGULIZI

**M**ei Mosi ni Siku ya Maadhimisho ya Wafanyakazi Duniani, na inaungwa mkono na Shirika la Kazi la Dunia (ILO). Wafanyakazi huadhimisha siku hii kwa kuwakumbuka Wafanyakazi waliopoteza maisha yao katika kupigania Haki na Maslahi ya Wafanyakazi.

## 2. HISTORIA YA MEI MOSI

Mwishoni mwa karne ya 19 tabaka la Wafanyakazi nchini Marekani lilikuwa katika mapambano makali na Waajiri ya kupigania kupunguza saa za kufanya kazi. Wafanyakazi walilazimika kufanya kazi kwa saa 10 mpaka saa 16 kwa siku; katika mazingira mabaya kabisa.

Vifo na kuumia kazini ilikuwa ni jambo la kawaida kwa Mfanyakazi.

Miaka ya mwanzo ya 1860, Wafanyakazi walianza kushinikiza saa za kazi zipunguzwe, bila kuathiri kipato cha Mfanyakazi. Shinikizo hili lilipata nguvu zaidi miaka ya 1880 ambapo Wafanyakazi waliunda umoja wao (Vyama) na kutangaza saa za kazi kuwa 8 kwa siku. Waajiri kwa upande wao hawakukubaliana na suala hili.

Mkutano Mkuu (National Convention) wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Marekani (Federation of Organised Trades and Labour Unions) ambalo baadaye lilikuja kujulikana kama American Federation of Labour (AFL) kwa kauli moja wajumbe waliazimia na kutamka kuwa ifikapo tarehe 1 Mei, 1886 saa za kazi kwa

Wafanyakazi wa Marekani zitakuwa 8 tu kwa siku. Mwaka 1887 Shirikisho hili liliazimia kuwa tamko la saa 8 za kazi kwa siku litaungwa mkono kwa kuitisha migomo na maandamano ya Wafanyakazi.

Mwaka 1889 Mkutano wa Kimataifa wa Soshalisti (2<sup>nd</sup> International Socialist Conference), uliofanyika Paris – Ufaransa ulitangaza rasmi kwamba Mei Mosi ni Sikukuu ya Wafanyakazi wote Duniani, itakayoadhimishwa na Wafanyakazi wote.

Wafanyakazi wengi chini ya uongozi na usimamizi wa Vyama vya Wafanyakazi Marekani waliunga mkono tamko hili na kulitekeleza kwa kufanya kazi kwa saa 8 kwa siku.

Mei Mosi ya kwanza nchini Marekani tarehe 1 Mei, 1887 zaidi ya Wafanyakazi 300,000 kutoka zaidi ya sehemu 13,000 za kazi waliamua kugoma. Mjini Chicago, ambapo palikuwa ndio chimbuko la saa 8 za kazi kwa siku, Wafanyakazi 40,000 walifanya mgomo na maandamano katika mitaa mbalimbali ya jiji hilo. Idadi hii iliongezeka hadi kufikia 100,000. Wafanyakazi wengi walipigwa na Polisi na kuumizwa na wengine wengi kuuwawa.

Historia hii inatuonyesha kwamba wafanyakazi wengi walipigwa na wengine kuuwawa kwa kudai kufanya kazi saa 8 kwa siku. Wengine wengi walichomewa nyumba zao kwa kudai Jumamosi iwe siku ya mapumziko, na watoto walioandamana kupinga



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu Mhe. Jenister Mhagama, Waziri wa Viwanda Mhe. Mwijage wakishiriki katika kongamano la Tanzania ya Viwanda lililoandaliwa na TUICO Tarehe 27/04/2018 mjini Iringa.*



Ajira ya Watoto walipigwa na Polisi na Waajiri wao.

Hii inatukumbusha kuwa hali ya wafanyakazi ilivyo sasa duniani inatokana na haya mapambano yaliyoendeshwa na wafanyakazi na vyama vyao enzi hizo ya kudai HAKI NA MASLAHI yao. mapambano haya hayawezi kusahaulika na tutayaendeleza mapambano hayo wakati wote. Hii ndiyo sababu kubwa ya kukutana na kusherehekea Mei Mosi duniani wakati wote.

### 3. CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WAFANYAKAZI

Tabaka la wafanyakazi duniani linakabiliwa na changamoto mbalimbali. Hii ni kutokana na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia yaliyopo duniani muda huu. Changamoto hizo ni pamoja na:-

#### (i) Ukosefu wa Ajira

Wapo vijana wengi wanaohitimu mafunzo kila mwaka, lakini hawapati ajira. Wengi wapo mitaani na wengine wameingia kwenye sekta ya uchumi isiyo rasmi.

#### (ii) Vipato duni

Kwa wale walio katika ajira wafanyakazi wengi hulipwa kipato kidogo ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji yao ya kila siku kwa mwezi mmoja.

#### (iii) Mazingira ya kazi yasiyofaa

Wengi wanafanya kazi kwenye mazingira hatarishi.

Hawapewi vifaa sahihi vya kinga na vya kufanyia kazi.

#### (iv) Waajiri wakorofi wasiopenda Wafanyakazi wajiunge na Chama

Pamoja na kwamba Sheria inaruhusu wafanyakazi kujiunga katika Vyama vya Wafanyakazi, baadhi ya Waajiri wanazuia wafanyakazi kujiunga na kutishiwa kufukuzwa kazi.

#### SALAAM

Chama kinatoa salaam katika maadhimisho haya ya Mei Mosi, kikiwatakia maadhimisho mema Wafanyakazi wote. Pia chama kinawahimiza kufanya kazi kwa bidii ili taasisi zenu zifanye vizuri na hatimaye kuboresha maisha yenu

**“Jenga Chama Imara na Imarisha Mshikamano”**



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Ndg. Amos Makala akiwa pamoja na Katibu wa TUICO Mkoa Ndg. W. Kapinga wakitoa vyeti kwa wafanyakazi bora.

# DHANA YA AFYA NA USALAMA KAZINI

**Na: Silpha Kapinga,  
TUICO Makao Makuu.**

## UTANGULIZI

**U**salama na Afya Kazini (OHS) ni azma mahususi inayolenga kulinda Usalama, Afya na Ustawi wa watu wote walio katika ajira iliyo rasmi.

Suala la Usalama na Afya Kazini linajumuisha pia kuwakinga/kuwalinda wafanyakazi wengine wanafamilia, waajiri, wateja, watoa huduma pamoja na jamii iliyozunguka ambao kwa njia moja au nyingine wanaweza kudhurika na mazingira ya sehemu ya kazi.

## USALAMA NA KAZI

Usalama unajumuisha mazingira huru yasiyo na ajali, mikwaruzo ya mwili na kudondokewa na vitu. Usalama Kazini unaweka mazingira huru ya kutokuwa na ajali.

Mikwaruzo ya mwili au vitu vidondokeavyo watu ndio vilivyozoeleka kutambulika kuwa ni madhara ya kutokuwa na usalama kwenye maeneo ya kazi. Pia maumivu yatokanayo na michubuko au mikwaruzo ni matokeo ya mara mtu aumiapo au ni madhara yanayotarajiwa baada ya mfanyakazi kuumia.

Wafanyakazi wengi pia hupata madhara makubwa na hata kufa endapo vitu vyenye ncha kali au vitu vinavyofanana na hivyo vimwangukiapo kichwani ikiwa mfanyakazi hakuvaa vifaa vya kinga (Protective gears).

Hivyo usalama kazini inadhamiria kuweka mazingira huru ya kutopata ajali ambayo yangesababisha madhara kwa mfanyakazi. Usalama huhusisha kudhibiti nguvu za



*Mtendaji wa TUICO Ndg. T. Mkolokoti akiwahamasisha Wafanyakazi kujiunga na TUICO.*

ziada katika maeneo ya kazi kwa mfano:-

- Mvuto wa nguvu za ziada
- Nguvu ya uwezo wa uzalishaji (kwa mtu)
- Nguvu ya vitu
- Nguvu za mashine
- Nguvu za magari na jumuiya (watu)
- Nguvu za umeme
- Nguvu za moto na joto
- Nguvu za kemikali n.k.

Ni dhahiri kuwa mtu huweza kukingwa / kuepushwa na madhara haya. Kama mwili wa mwanadamu utakuwa umewekwa katika mazingira hatari kwa kiwango kikubwa, matokeo yake ni madhara makubwa yatakayosababisha ulemavu au ajali mbaya.

Afya hujumuisha kutokuwa na maradhi yoyote mwilini. Maradhi yanaweza kusababishwa na maambukizi mbalimbali kutoka kwenye vimelea vya kibaiolojia, lakini pia yanaweza kuwa ni matokeo ya kuwa katika mazingira hatari kwa kazi za kila siku

kwa muda mrefu. Kwa mfano:-

- Kemikali
- Kelele, joto, mionzi
- Matumizi ya mitambo na madhara ya kiigonomia
- Visababishi vilivyo katika jamii

Endapo nguvu kubwa itatumika wakati wa kutumia kemikali (mfano wakati wa kumwaga kemikali), madhara ya moja kwa moja huweza kutokea.

Hivyo kwa kawaida matumizi ya nguvu kidogo huhitajika katika tathimini ya udhibiti unaofaa kuhakikisha madhara na magonjwa yanayoweza kutokea yanapunguzwa.

## MALENGO YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Afya na Usalama hulenga yafuatayo:-

- Kuweka na kuboresha mazingira mazuri yatakayopelekea ustawi wa wafanyakazi wote kimwili na kiakili.



- Kuwakinga wafanyakazi na madhara yatokanayo na Afya na Usalama yanayoweza kuwasababishia kuacha kazi.
- Kuwakinga wafanyakazi katika ajira zao kutokana na madhara ya kiafya yanayoweza kuwakabili
- Kuweka na kuhakikisha mfanyakazi anayaelewa na kuyakabili maeneo yake ya kazi kimazingira na kisaikolojia.



Washiriki kutoka Sekta Isiyorasmi (Bajaj, Bodaboda, Mama na Baba Lishe) wakifuatilia kwa makini mafunzo yaliyoendeshwa na TUICO katika maadhimisho ya Mei Mosi kitaifa 2018 Iringa.

### **Kwanini TUICO imeanzisha mpango wa kuimarisha Afya na Usalama Kazini?**

Sababu za kuanzisha mpango wa Usalama na Afya Kazini ni kama ifuatavyo:-

#### • **Maadili**

Mfanyakazi hapaswi kuwa katika mazingira yatakayohatarisha maisha yake binafsi awapo kazini na hata wengine wanaomzunguka.

#### • **Kiuchumi**

Serikali nyingi zinatambua kwamba Usalama na Afya duni kazini unapelekea hasara kwa Taifa. (mfano, Serikali huingia gharama kuwatibu, kuwahudumia majeruhi, kuwalipa fidia na mfanyakazi kushindwa kufanya kazi tena).

#### • **Kisheria**

Mahitaji ya Afya na Usalama Kazini yameainishwa na Sheria ya Madai na Sheria ya Jinai. Bila shaka pasipokuwa na msisitizo wa kisheria sehemu nyingi za kazi hazitaweza kutekeleza majukumu yake ya kuimarisha suala la Usalama na Afya kwa Wafanyakazi ipasavyo.

### **AINA ZA MADHARA YA AFYA NA USALAMA**

Madhara ni tukio (inajumuisha nguvu au hali ya mazingira) ambayo inaweza kusababisha majeraha/maumivu au maradhi kwa mtu (uharibifu wa mazingira, uharibifu wa vitu n.k.).

Zifuatazo ni aina za madhara yatokanayo na Usalama na Afya Kazini:-

- Madhara ya kiumbo
- Madhara ya kibaiolojia
- Madhara ya Kemikali
- Madhara ya Kisaikolojia
- Madhara ya Kiigonomia
- Madhara ya mpangilio mpya wa kazi
- Madhara ya mazingira.
- VVU/UKIMWI

### **MUUNDO WA SHERIA NA ASASI**

#### **Viwango vya Shirika la Kazi Duniani**

Moja ya dhumuni la Shirika la Kazi Duniani tokea kuanzishwa kwake, imekuwa ni kusimamia Viwango vya Kimataifa vya Kazi na Ustawi wa Wafanyakazi.

Viwango hivi vya Kimataifa

vya Kazi hufanyika na kuwa na Mikataba na Maazimio ya kiutendaji baina ya nchi Mwanachama na Shirika. Karibu Mikataba na Maazimio 70 ya kiutendaji baina ya nchi Wanachama yanahusu masuala ya Usalama na Afya Kazini.

Pamoja na Mikataba na Maazimio ya Shirika la Kazi Duniani kuhusisha masuala ya Afya na Usalama Kazini, kuna Sheria mbalimbali na Miongozo inayotolewa ili kusimamia Usalama na Afya Kazini kutoka kwa uongozi wa nchi husika.

### **AZIMIO NAMBA 187 LA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI**

Azimio la kudumisha na kuimarisha Usalama na Afya Kazini. Kila mwanachama anayeridhia Azimio hili:-

- Atapaswa kuanzisha na kuendeleza masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi ili kuzuia ajali, maradhi na vifo.
- Lazima kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora kupitia Mitandao na Miongozo ya Kitaifa inayohusu Usalama na Afya Kazini.



- Kwa ushirikiano wa Uwakilishi wa Waajiri na Wafanyakazi watapaswa kupanga muda wa kukutana na kujadili mapendekezo mbalimbali kuhusu kurekebisha/kuboresha hali za Usalama na Afya Kazini kulingana na Maazimio ya Shirika la Kazi Duniani.

### **Mpango wa Taifa wa Afya na Usalama utahusisha mambo yafuatayo:-**

- Sheria na Mwongozo, Mikataba ya Hiari inapohusika na nyongeza zingine zihusikanazo
- Mamlaka, chombo au vyombo viundwavyo kufuatana na Sheria za nchi vitakavyoshughulikia masuala ya Usalama na Afya.
- Mpango utakaohusisha kufuatwa kwa Sheria za nchi, ikiwemo mifumo ya ukaguzi
- Utoaji wa mafunzo ya Utafiti wa masuala ya Usalama na Afya.

### **SHERIA YA AFYA NA USALAMA KAZINI TANZANIA**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka Sheria ya Afya na Usalama Kazini.

Sheria hii inatambulika kama Sheria ya Afya na Usalama Kazini Na. 5 ya mwaka 2003., inatoa muongozo kuhusu madhumuni kwa ujumla na mahitaji muhimu kwa sehemu za kazi.

Sheria hii inalenga katika kuzuia ajali na magonjwa sehemu za kazi ikiwa ni pamoja na kuwakinga Wafanyakazi kutokana na madhara mbalimbali sehemu za kazi kama yalivyoainishwa katika vipengele mbalimbali ndani ya Sheria.

### **Vipengele muhimu katika Sheria hii ni:-**

Mwongozo wa Sheria ya Afya na Usalama sehemu ya kazi kama:-

- Wawakilishi wa Afya na Usalama sehemu ya kazi (Kif.11)
- Kazi za Wawakilishi wa Afya na Usalama (Kif.12)
- Kamati za Afya na Usalama (Kif.13)
- Kazi za Kamati za Afya na Usalama (Kif.14)

### **Usajili wa maeneo ya kazi**

Sheria inatoa mwongozo wa jinsi ya kujisajili.

### **Mahitaji ya kiusalama sehemu za kazi**

- Uchunguzi wa Afya
- Vifaa vya Kinga
- Usafi wa mashine
- Viwango vya ubebaji
- Vifaa vya kunyanyulia vitu

### **Utoaji wa mahitaji ya Afya na Ustawi wa Jamii**

- Maji ya kunywa
- Vifaa ya kuoshea
- Vifaa ya huduma ya kwanza

### **Kuweka usalama unajumuisha**

- Kuondoa vumbi
- Kuweka vifaa vya kinga
- Kukinga macho n.k.

### **Matumizi ya Kemikali huhusisha:**

- Hatua za udhibiti kwa ujumla wakati wa kutumia kemikali.

### **Makosa, adhabu na taratibu za kisheria**

- Kushindwa kutekeleza matakwa ya Sheria hii kutapelekea adhabu kwa upande uliotenda kinyume.

### **SERA YA TAIFA YA AFYA NA USALAMA KAZINI**

Kwa mujibu wa malengo ya muda mrefu ya Tanzania kupunguza umaskini kwa Wananchi na kuendeleza masharti ya kazi katika maeneo yote ya kazi, kwa kutoa viwango bora vya Afya na Usalama Kazini, Serikali imeanzisha Sera ya Taifa ya Afya na Usalama.

Malengo ya Sera hii ni kukinga na kudhibiti ajali kazini, magonjwa na kuumia ili kudumisha Afya na Ustawi wa Wafanyakazi na kuongeza Tija.



*Mtendaji wa TUICO - Temeke akiwa na Wanachama na Viongozi wa TUICO Matawini.*

# M A T U K I O K A



Raisi wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) Ndg. Tumaini Nyamhokya akibadilishana mawazo na Mwenyekiti wa TUICO-Taifa Mhe. Paul Sangeze.



Banda la maonesho la TUICO katika kuadhimisha sherehe za Afya na Usalama Kazini mkoani Iringa.



Katibu wa TUICO Kanda, Ndg. Merboth Kapinga akitoa shukrani kwa niaba ya Wajumbe wa Kanda 16/02/2018.



Raisi wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) Ndg. Tumaini Nyamhokya akifungua Semina ya Matawi ya TUICO Mkoani Iringa katika maadhimisho ya Mei Mosi kitaifa.



Watendaji wa TUICO-Temeke wakiwa katika uchaguzi wa viongozi wa tawi la Man Track.



Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake TUICO Mkoa Ndg. Joice Lambwe akikabidhi mashuka ya wagonjwa kwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Meta, Mbeya 07/03/2018.



# T I K A P I C H A



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wakiwa kwenye picha ya pamoja na Uongozi wa Kiwanda cha Bia Tanzania, 16/02/2018.*



*Raisi wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) Ndg. Tumaini Nyamhokya (Wa pili kushoto), Mwenyekiti wa TUICO-Taifa Mhe. Paul Sangeze (Wa tatu kulia) wakiwa na watendaji wa TUICO pamoja na Wanasemina, Iringa.*



*Washiriki wa Semina ya Wajasiriamali wa Boda boda, Bajaj, Mama na Baba Lishe wa mkoani Iringa. Semina hiyo iliendeshwa na TUICO katika maadhimisho ya Mei Mosi Kitaifa mkoani Iringa.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank PLC Dr. Charles Kimei akibadilishana mkataba wa hali bora za kazi na Mkuu wa Sekta ya fedha TUICO Makao Makuu Ndugu Willy Kibona, 15/02/2018.*



*Viongozi wa Kabila la Wahehe wakishiriki kikamilifu maadhimisho ya Meimosi Kitaifa 2018 Iringa.*



*Washiriki wa kongamano la Tanzania ya Viwanda lililoandaliwa na kuratibiwa na TUICO katika maadhimisho ya Mei Mosi kitaifa Iringa Tarehe 27/04/2018.*

# WAJIBU NA HAKI ZA VIONGOZI WA TUICO KWA MWAJIRI KATIKA UBORESHAJI WA UTENDAJI KAZI

**Na: Willy Kibona,**  
**TUICO Makao Makuu.**

## Utangulizi

**W**ajibu na haki za Viongozi wa TUICO kwa Mwijiri katika uboreshaji wa Utendaji kazi ni pamoja na:-

- Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya Wafanyakazi kazini
- Kushirikiana na kujadiliana na Waajiri kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi
- Kudumisha amani mahali pa kazi
- Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza mahali pa kazi
- Kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Hali Bora za Kazi
- Kusimamia utekelezaji wa TUZO, Kanuni za Utumishi na Sheria nyingine za Kazi
- Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na Vyama vingine vya Wafanyakazi
- Kuwasiliana na Serikali kuhusu hoja ya kutunga Sheria sahihi za kazi na kuandaa Sera nzuri za kuendeleza uchumi na maisha ya jamii
- Kulinda maslahi ya Wafanyakazi

## Haki za Viongozi wa TUICO kwa Mwijiri

Majukumu na Haki za Viongozi wa TUICO kwa mujibu wa kifungu cha 62(4) cha Sheria ya



*Viongozi wa Kamati ya Majadiliano CRDB Bank PLC na TUICO wakitia saina Mkataba wa Hali Bora, Mwezi Februari 2018.*

Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Katiba ya TUICO Ibara ya 7.4.1. ni pamoja na:-

- Kuwawakilisha Wanachama kwenye malalamiko, vikao vya nidhamu na migogoro ya kikazi
- Kushauriana na Mwijiri juu ya uzalishaji, kukuza tija na kuendeleza ajira
- Kukiwakilisha Chama kwenye masuala ya ukaguzi na uchunguzi kwa mujibu wa Sheria za Kazi
- Kutoa hoja kwa niaba ya Wanachama juu ya Kanuni za Afya, Usalama na Ustawi
- Kuhamasisha na kuingiza Wanachama wanya
- Kusimamia Mapato na Matumizi ya fedha za Chama katika Tawi

- Kutunza kitabu cha kumbukumbu cha Wanachama
- Kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Chama kwa Katibu wa Mkoa
- Kuendeleza uhusiano bora na Mwijiri mahali pa kazi
- Kushirikiana na Katibu Mkuu au Mwakilishi wake katika Majadiliano ya pamoja na Mwijiri
- Kuhakikisha Wanachama wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa Katiba
- Kutoa taarifa kwa Katibu wa Mkoa juu ya mgogoro wa kikazi unaoweza kusababisha kuzorota kwa kazi kwa hatua zaidi.
- Kupokea, kuwasilisha, kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya ngazi za juu za Chama.



- Kuendeleza uhusiano bora na matawi mengine
- Kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa na Mwajiri

### Kusimamia Tija na Ufanisi

Uboreshaji na utendaji kazi unaoleta tija kiongozi wa TUICO anatakiwa kufanya yafuatayo:-

- Kuhakikisha malalamiko ya Wafanyakazi sehemu ya kazi yanatatuliwa kwa wakati
- Kuhakikisha Kanuni za Ajira zinaeleweka na kutekelezwa
- Kuhakikisha mipango ya kukuza uchumi wa taasisi ipo
- Kuhakikisha Mwajiri anatoa vifaa vya kazi kwa wakati
- Kuendeleza uhusiano bora mahali pa kazi
- Kuelimisha Wafanyakazi namna ya kuepuka migogoro kazini
- Kuhakikisha taratibu za kazi zinazingatiwa na wahusika wote

- Kuwa kiungo kati ya Wafanyakazi na Menejimenti

Masuala ya kiutendaji na TUICO ili kuondoa migogano kazini

- Masuala ya kiutendaji ni mambo mbalimbali yaliyoainishwa kwenye Sheria, Kanuni, Sera mbalimbali ambayo yamepitishwa na Mamlaka husika ili kufanikisha Malengo ya Taasisi.
- Masuala ya kiutendaji husimamiwa na Menejimenti ili kufanikisha utekelezaji wake, kwa mujibu wa maelekezo ya mamlaka ya juu
- Wajibu wa TUICO ni kuhakikisha kuwa hakuna ukiukwaji wa haki na maslahi ya Wafanyakazi katika utekelezaji wa masuala ya kiutendaji.

### Tofauti

- Menejimenti inatekeleza masuala ya utendaji ili

kufanikisha malengo na nidhamu kazini

- TUICO inahakikisha kuwa wakati wa utekelezaji hakuna athari kwa Wafanyakazi ili kupata tija
- Menejimenti inawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji kwa mamlaka ya juu
- TUICO inawajibika kushauri namna nzuri ya utekelezaji wa suala husika na kuelimisha Wafanyakazi juu ya faida na athari zake
- Masuala ya kiutendaji ni ya Kikanuni zaidi, jukumu kubwa ni kwa Menejimenti kufanikisha
- TUICO husimamia na kuona kuwa masuala hayo hayaleti madhara kazini.

### Namna ya kujenga na kuwasilisha hoja

- Hoja lazima iwe na misingi ya Sheria, Kanuni, Sera au Mikataba
- Hoja lazima iwe na Mmiliki
- Hoja lazima iwe na nguvu ya ushawishi (nguvu ya hoja na siyo Hoja ya Nguvu)
- Hoja iwe imefanyiwa utafiti wa kina kabla ya kuwasilishwa
- Hoja ibebe malengo ya Taasisi na maslahi ya wengi
- Muwasilishaji wa hoja asiwe na mtizamo hasi juu ya upande mwingine wakati wa uwasilishaji
- Hoja ziandaliwe mapema na kuwasilishwa kwa wakati unaofaa



Picha ya pamoja ya Wajumbe wa Kamati ya Wanawake TUICO wakiwa na Viongozi wa Hospitali ya Meta, Mbeya, kwenye siku ya Wanawake Duniani 07/03/2018.

# MIKATABA YA AJIRA

**Na: Silpha Kapinga,  
TUICO Makao Makuu.**

## 1.0. MAANA

- (i) Mwajiri maana yake ni mtu yeyote ikiwemo Serikali na Wakala ambaye anaajiri Wafanyakazi
- (ii) Chama cha Waajiri maana yake ni Waajiri waliojiunga pamoja kwa ajili ya kurekebisha mahusiano baina ya Waajiri na Waajiriwa au Chama cha Wafanyakazi kinachowakilisha Wafanyakazi
- (iii) Mwajiriwa ina maana mtu ambaye:-
  - (a) Ameingia mkataba wa ajira au
  - (b) Ameingia katika mkataba mwingine wowote ambao
    - Anafanya kazi mwenyewe kwa niaba ya upande mwingine katika mkataba, na
    - Upande mwingine sio mteja wa taaluma yeyote, biashara au shughuli yoyote inayofanywa na mtu huyo au
    - Anachukuliwa kuwa mwajiriwa na

Waziri chini ya kifungu cha 98 (3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini

## 1.1. AINA ZA MIKATABA YA AJIRA

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 inaagiza kuwe na mikataba ya ajira kwa mtu yeyote anayeajiriwa mahali popote.

Zipo aina tatu za Mikataba ya Ajira kwa mujibu wa Sheria hii:-

- (i) Mkataba wa muda usiokuwa maalum
  - (ii) Mkataba wa muda maalum kwa wataalamu na Viongozi walio katika kada ya uongozi
  - (iii) Mkataba wa kazi maalum
- Mkataba wa mwajiriwa utakuwa katika maandishi, kama mkataba utaeleza kwamba mwajiri atafanya kazi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## 1.2. WAJIBU WA MWAJIRI

- (a) Mwajiri analazimika kumpatia Mwajiriwa wakati anaanza kazi taarifa ya kina ya maandishi yenye kuonyesha:-
  - (i) Jina, umri, anuani ya kudumu na jinsia ya mwajiriwa
  - (ii) Mahali ajira ilipofanyika

- (iii) Maelezo ya kazi tarajiwa
  - (iv) Tarehe na siku ya kuanza ajira
  - (v) Aina na muda wa mkataba
  - (vi) Mahali pa kazi
  - (vii) Saa za kazi
  - (viii) Kiwango cha malipo (Mshahara na marupurupu mengineyo atakayolipwa kama yapo)
  - (ix) Mambo mengine yaliyoeleza
- (b) Kama Mwajiriwa hataelewa maelezo ya maandishi, Mwajiri anapaswa kuhakikisha kwamba maelezo haya yanafafanuliwa kwa Mwajiriwa kwa namna ambayo Mwajiriwa ataelewa.
  - (c) Ikitokea mambo yaliyoeleza hapo juu yamebadilika, Mwajiri atatakiwa kumuarifu Mwajiriwa kuhusu mabadiliko hayo kwa maandishi.
  - (d) Mwajiri atatunza maelezo ya maandishi yahasuyo Mkataba wa Ajira wa Mfanyakazi wake kwa muda wa miaka mitano baada ya kumwachisha kazi.
  - (e) Katika mgogoro au shauri lolote la kisheria Mwajiri akishindwa kuonesha/kuwasilisha taarifa ya Mwajiriwa ya maandishi anayopewa Mwajiriwa wakati wa kuanza kazi, jukumu la kuthibitisha au kutohibitisha madai



ya Mwajiriwa linabaki kwa Mwajiri.

- (f) Kila Mwajiri anapaswa kubandika haki za Mfanyakazi kwenye ubao wa Matangazo ambapo kila mmoja anaweza kusoma.

Masharti ya mkataba wa ajira yaliyotajwa hapo juu hayatatumika kwa Mwajiriwa aliyefanya kazi chini ya siku sita kwa mwezi kwa Mwajiri.

Maelezo haya yote yanatokana na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 kifungu cha 14 na kifungu cha 15 kwa ujumla wake.

## 2.0. UBAGUZI MAHALI PA KAZI

### Maana ya Ubaguzi

Ubaguzi ni neno linalotumika kueleza tabia zinazooneshwa na Waajiri au mtu yeyote kuwetenga Wafanyakazi kwa misingi mbalimbali kama vile rangi, jinsia, umri, VVU/UKIMWI au kwa kigezo kingine chochote katika Sera za Ajira au taratibu zilizopo/zilizozoeleka.

### 2.1. Maana ya Sera za Ajira

Sera za Ajira au taratibu za kazi ni pamoja na:-

- Taratibu za ajira
- Vigezo vya utangazaji wa nafasi za ajira na uteuzi
- Mgawanyo wa kazi na madaraka
- Mishahara
- Mafao ya ajira, muda na masharti ya ajira
- Mazingira ya kazi na sukula (facilities) ugawaji wa kazi
- Mafunzo na maendeleo
- Mifumo ya tathimini ya utendaji, upandishaji vyeo na uhamisho.

### 2.2. Majukumu ya Mwajiri

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 inamtaka Mwajiri ahakikishe anakuza fursa sawa katika ajira na kupambana kutokomeza ubaguzi katika Sera yoyote ya ajira au katika utendaji (Kifungu cha 7(1).

### 2.3. Aina za Ubaguzi

#### (a) Ubaguzi wa moja kwa moja

Hii inatokea pale Mwajiriwa anapotendewa ubaguzi kwa kufuata vigezo vya rangi, utaifa, kabila, Mbari, msimamo wa kisiasa, umri, jinsia, ulemavu.

#### (b) Ubaguzi usio wa moja kwa moja

Ubaguzi huu hutoka pale mahitaji au masharti ambayo mbele yake yanaonekana kuwa ya kawaida yana athari za kubagua mtu au kada ya watu kwa vigezo vilivyotajwa hapo juu.

Mfano unatoa tangazo la kazi kwenye gazeti ambalo linafika kwenye mkoa mmoja tu (Morogoro, kwa mfano) ingawa itaonekana kuwa tangazo hili lipo sawa lakini limebagua watu walio katika mikoa mingine kwa sababu hawataweza kuliona.

Aina nyingine ya ubaguzi ni pamoja na ubaguzi uliopangiliwa, ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa kidini.

### 2.4. Vitendo visisyo vya kibaguzi si ubaguzi

- (a) Kuchukua hatua za

makusudi za kukuza usawa na kuondoa ubaguzi mahali pa kazi.

Mfano unatoa tangazo la kazi na kuweka kipengele kitakachowachochea wanawake kutuma maombi.

Hizi ni jitihada za makusudi zenye lengo la kuongeza idadi ya Wafanyakazi Wanawake kwenye eneo la kazi.

- (b) Kutofautisha, kuondoa au kumpelekea mtu yeyote kwa msingi wa masharti ya kazi mfano kama unahitaji dereva, tangazo lako la kazi ni wazi litawabagua wenye ulemavu wa mikono, miguu au wenye mtindio wa ubongo.
- (c) Kuajiri wananchi kulingana na Sheria ya Taifa ya kukuza Ajira.

### 2.5. Majukumu ya Waajiri

- (a) Kuandaa na kuchapisha mpango wake wa kuzuia ubaguzi mahali pa kazi na kukuza fursa sawa katika ajira.

Katika mchakato wa kuandaa mpango huu, Mwajiri ashauriane na Chama cha Wafanyakazi, na pale ambapo hakuna Chama, Mwajiri awaalike Wawakilishi wa Wafanyakazi kushiriki katika kuandaa mpango huu.

- (b) Kimsingi ni jukumu la Mwajiri kuhakikisha kuwa kunakuwepo fursa sawa kwa wote mahali pa kazi.

- (c) Mwajiri atapitisha, atawasilisha, atatekeleza, atafuatilia na kupitia upya mara kwa mara Sera za kuandoa ubaguzi.
- (d) Katika kutangaza nafasi za ajira Mwajiri ataepuka kutotenda haki kwa kutoa matangazo ya kazi kwa maeneo au machapisho ambayo yanaweza kuwatenga au kupunguza kutowiana idadi ya waombaji.
- (e) Kuchambua vigezo vya uteuzi na majaribio, mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa vinahusiana kikamilifu na masharti ya kazi na havibagui waombaji moja kwa moja au kwa njia nyingine.
- (f) Kuhakikisha kuwa shughuli ya kufanya uteuzi wa awali na kusaili waombaji usifanywe na mtu mmoja na pia ikaguliwe na mtu mwingine ambaye ni kiongozi mwandamizi.
- (g) Kuhakikisha kuwa vigezo vya kuchagua wafanyakazi kwa ajili ya mafunzo, iwe kwa kuingia kazini, kupandisha vyeo au mafunzo ya kiufundi si vya kibaguzi.
- (h) Kila Mwajiri achunguze Sera zake kila mara ili kuepuka ubaguzi usio wa moja kwa moja
- (i) Kila Mwajiri ahakikishe kuwa wale wanaowajibika kufanya tathimini na mapitio ya utendaji kazi hawabagui.

## 2.6. Majukumu ya Mwajiriwa

Ili kujenga na kukuza mazingira ya kazi yasiyo ya kibaguzi Mwajiriwa anapaswa:-

- (i) Kumjulisha Mwajiri au Chama cha Wafanyakazi kinachotambulika juu ya tabia yoyote ya kibaguzi
- (ii) Kuepuka kuwafanyia vurugu au kuwashambulia wafanyakazi wengine.

## 2.7. Majukumu ya Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi

- (a) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuandaa mpango wa kuzuia ubaguzi na kukuza fursa sawa katika ajira.
- (b) Kukuza fursa sawa na kujenga mahusiano mazuri mahali pa kazi
- (c) Kuwasiliana / kushauriana na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa katika masuala yote yatakayosaidia kuzuia ubaguzi mahali pa kazi.

## 2.8. Majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi

- (a) Maafisa wa Vyama na Wawakilishi wa Chama cha Wafanyakazi wana nafasi muhimu kwa niaba ya Wanachama wao katika kuzuia ubaguzi na katika kukuza fursa sawa na uhusiano mzuri katika ajira
- (b) Vyama vya Wafanyakazi visibague kwa kumkataa Mwanachama kwa sababu zozote zile za kibaguzi

(c) Kutoa mafunzo na taarifa kwa maofisa na kuwakumbusha kuhusu wajibu wao kwa ajili ya fursa sawa

(d) Kushirikiana na Waajiri katika kuondoa, kutekeleza na kufuatilia mipango ya kuondoa ubaguzi na kukuza usawa.

## 2.9. Madhara ya Ubaguzi

Madhara yatokanayo na kubagua Wafanyakazi yameainishwa katika kifungu cha 102 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Kifungu hiki kinaelekeza kuwa Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakim Mkazi inao uwezo wa kutoa adhabu kwa Mwajiri atakayekiuka Sheria hii na hivyo kutenda kosa.

Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa makosa yaliyoanishwa katika kifungu cha 7, 8, na 9 cha Sheria hii anaweza kuhukumiwa kulipa faini isiyozidi Shilingi milioni moja za Kitanzania.

## 3.0. HITIMISHO

Ni jukumu la Waajiri, Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi ni kuhakikisha kuwa ubaguzi wa aina yoyote sehemu ya kazi haupevi nafasi.

Uhusiano mzuri sehemu ya kazi ni jambo muhimu katika kuongeza tija na kukuza ushirikiano na uelewano kazini.

Wadau wote wanapaswa kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote.



# UCHUMI WA VIWANDA KUZINGATIA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI

**Na: Silpha Kapinga,  
TUICO Makao Makuu.**

**K**atika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Afya na Usalama Duniani, ambayo kitaifa yalifanyika Mkoa wa Iringa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi Vijana Ajira na Wenye Ulemavu) Mh. Jenista Mhagama alipokuwa akihutubia wananchi na wageni mbalimbali waliohudhuria alisema “katika kipindi hiki ambapo mwelekeo wa nchi ni kujenga uchumi wa viwanda, suala la Afya na Usalama wa Wafanyakazi ni lazima lizingatiwe”.

Alisisitiza kuwa “Serikali ya awamu ya tano kamwe haitapuuzua suala la Usalama na Afya mahala pa kazi hasa wakati huu tunapojenga uchumi wa viwanda ambao utaambatana na vihatarishi vingi vipya”, aliongeza kuwa “kwa hiyo Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ili kupunguza au hata ikiwezekana kuondoa kabisa vifo, ajali, magonjwa na madhara yatokanayo na kazi”.

Kwa hapa nchini masuala ya Afya na Usalama katika sehemu za kazi, yapo chini ya Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA) ambao husimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Bunge ya Afya na Usalama mahali pa kazi ya mwaka 2003. OSHA husajili sehemu zote za kazi nchini na kuzitembelea kwa ajili ya kufanya kaguzi za kiusalama na afya ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na mifumo madhubuti ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi mbalimbali vitokanavyo na kazi wanazozifanya.

Vivyo hivyo Chama cha Wafanyakazi cha TUICO kimeunda Kamati za Afya na Usalama mahala pa kazi katika maeneo mengi ya kazi, ambazo zinashirikiana na mwajiri na chama katika kuboresha mazingira ya kazi kuwa salama.

Hivyo basi Waajiri kote nchini wametakiwa kutimiza wajibu wao wa kisheria kwa wafanyakazi

waliowaajiri kwa kuhakikisha kuwa wanaweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kuwapatia vitendea kazi muhimu vya kuwakinga na madhara ya kiafya katika maeneo ya kazi.

Ukweli ni kwamba wafanyakazi wamekuwa wakitumia muda mwingi kwa siku wakiwa mahali pa kazi kwenye viwanda, mashamba, afya, migodini, mabenki, maeneo ya kutolea huduma mbalimbali, pia wafanyakazi kwenye Sekta Isiyo Rasmi hivyo mazingira hayo lazima yawe salama kwa afya zao.

Wafanyakazi katika maeneo mbalimbali nchini karibu kila siku wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali zenye athari kwa afya zao, hasa athari za kibaiolojia, kikemikali, ajali za viungo vya miili yao, matatizo ya usikivu yanayotokana na mazingira yenye kelele na changamoto mbalimbali ambazo wakati mwingine husababisha vifo.

Hii siku ni kumbukumbu kwa wafanyakazi wote ulimwenguni waliopoteza maisha, walioumia wakiwa kazini, waliopata ulemavu, hivyo Vyama vya Wafanyakazi ni jukumu letu kuhakikisha tunawalinda wafanyakazi kutokana na ajali na magonjwa. Zaidi ya Wafanyakazi milioni 2.5 wanapoteza maisha kutokana na kuumia au kuugua kunakosababishwa na mazingira mabaya ya kazi kila mwaka.

Duniani kote mazingira duni/mabaya ya kazi yanaua wafanyakazi 11 katika kila sekunde na ni vifo ambavyo havizuiliki, na idadi ya vifo inaripotiwa kuongezeka.

Katika nchi yetu Vyama vya Wafanyakazi na Sheria za nchi zipo wazi na ni nzuri zinazolenga kuwalinda wafanyakazi. Kutakuwa na kampeni ya kidunia ya Usalama, Haki na Wajibu, hivyo basi ni jukumu la kila mmoja wetu kuona umuhimu wa kushiriki hii kampeni ili kupunguza madhara yatokanayo na mazingira mabaya ya kazi.

Ni muhimu zaidi wafanyakazi wakawa na uelewa pia kuhusu ugonjwawa Kansa unaosababishwa na kazi (Occupational Cancer) ambao unasababisha vifo zaidi ya milioni 2.4 kila mwaka; zaidi ya asilimia 10 ya kesi za kansa zinasababishwa na madhara yatokanayo na kemikali mahala pa kazi.

Vifo vitokanavyo na kansa mahala pa kazi ni tatizo kubwa na hasa maeneo ambayo wafanyakazi hawajahamasishwa kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi; hivyo kusababisha wadau mbalimbali kushindwa kutoa michango yao ipasavyo, hivyo ni jukumu letu Vyama vya Wafanyakazi kusaidia kufichua waajiri wasiozingatia Afya na Usalama mahala pa kazi; kuna mifano mingi ya maeneo ya kazi ambayo wafanyakazi wake walipata matatizo ya kansa sababu ya kuficha ukweli kuhusu mazingira ya kazi, mfano halisi ni Samsung Korea iliyoathirika kwa kemikali na mionzi ambapo ilikuwa ikifanya biashara kwa siri.

Sambamba na maadhimisho hayo, kulikuwa na bonanza la michezo kwa wafanyakazi kutoka maeneo mbalimbali ya kazi. Wanachama na wafanyakazi wanahimizwa sana kushiriki katika michezo mbalimbali ili kuboresha afya zao na kujikinga na maradhi mbalimbali kama magonjwa ya moyo na kisukari.

Hivyo basi Waajiri wote nchini wanahimizwa kuanzisha programu za michezo mahala pa kazi na kutoa nafasi kwa wafanyakazi kushiriki michezo, michezo inaimarisha mwili na kufanya ubongo ufanye kazi kwa ufasaha. Tujitahidi kuzingatia na kujali afya zetu.

Je, unatafuta chama kinachojali afya na usalama wako mahala pa kazi? Hujachelewa, jiunge na TUICO ufurahie maisha ukiwa kazini.

**“PREPARE AND PREVENT,  
DON’T REPAIR AND  
REPENT”**

# MGOGORO WA WAFANYAKAZI 453 WA MUFINDI PAPER MILLS (MPM)

**Na: Noel Nchimbi,**  
**TUICO Makao Makuu.**

## UTANGULIZI

Mufindi Paper Mills (MPM) ni Kiwanda cha kuchakata na kutengeneza Karatasi kilichopo mkoani Iringa Wilaya ya Mufindi, Kijiji cha Mgogolo.

Kiwanda hiki kilikuwa chini ya umiliki wa Serikali kikijulikana kama Southern Paper Mills (SPM) hadi ilipofika tarehe 14/2/2014 kilipobinafsishwa kwa Mwekezaji “Rai Group of Kenya” na kuitwa Mufindi Paper Mills.

## CHANZO CHA MGOGORO

Mgogoro ulianza pale mwekezaji alipogoma kuendeleza ajira za wafanyakazi wa iliyokuwa SPM kinyume na makubaliano baina ya Wafanyakazi, Mwekezaji na Serikali.

Mwekezaji alitaka Wafanyakazi waajiriwe upya, kwa maana waombe ajira upya na kuwapatia kipindi cha matazamio (Probation Periods), kitendo ambacho wafanyakazi waligoma na hivyo kugomea kazi ndipo tarehe 22/8/2005 Mwekezaji Rai Group aliwafukuza kazi wafanyakazi 453 kinyume na taratibu

## MASHAURI YA MGOGORO

Baada ya wafanyakazi kufukuzwa kazi pasipo kufuatwa kwa misingi ya Sheria za Kazi, wafanyakazi kupitia TUICO tulifungua mashauri mawili dhidi ya Serikali na Mwekezaji juu ya ukiukwaji wa Sheria na Taratibu kutozingatiwa kwa pande shindani na hatimaye Baraza la Usuluhishi chini ya Kamishna wa Kazi

mwezi Agosti, 2005 aliweza kuusikiliza mgogoro huu kwa mara ya kwanza, na baadae ukahamishiwa Mahakama ya Kazi.

Mnamo tarehe 29/11/2007 mgogoro huo ulipatiwa Tuzo mbele ya Mwanahaki Mheshimiwa Jaji Mwipopo, aidha Mahakama iliamuru kuwa wafanyakazi warudishwe kazini au waachishwe kazi kimaslahi (walipwe stahiki zao). Kutokana na Hukumu hiyo Mwajiri hakuridhika na uamuzi wa Mahakama hivyo akaomba Marejeo ya Hukumu hiyo.

Maamuzi ya Marejeo yalitolewa mwaka 2009 kwa kuwapa wafanyakazi tuzo kama ilivyotolewa na Mahakama ya Kazi. Baada ya marejeo hayo Mwajiri hakuridhika tena hivyo mnamo mwaka huo huo Julai, 2009 alikata rufaa ambayo ilidumu Mahakamni hadi Agosti, 2014 ilipotolewa hukumu nyingine.

Punde hukumu ilipotolewa, chama kililazimika kuanza kufuatilia Amri ya Utekelezaji wa hukumu ambapo ilitolewa tarehe 5/12/2016 na ndipo hapo sasa Mwajiri alikubali kukaa meza moja na Chama (TUICO) kuweza kujadiliana juu ya utekelezaji wa Tuzo iliyotolewa.

Majadiliano yalifanyika na hasa juu ya gharama nzima ya Tuzo hiyo ambapo Mwajiri alikuwa anadaiwa TShs.7,072,682,703/=. Mnamo tarehe 3/11/2017 chama pamoja na mwajiri tulifikia muafaka wa kuwa waliokuwa Wafanyakazi wa MPM walipwe jumla ya TShs. 5,000,000,000/= na fedha hizo zililipwa kwa awamu mbili, Novemba, 2017 na Januari, 2018.

## MAHUSIANO YA SASA BAINA YA MPM NA TUICO

Kwa sasa tumekuwa na mahusiano na mashirikiano mazuri sana baina ya MPM na TUICO. Shughuli za Chama mahala pa kazi zinaendelea bila vikwazo, uingizaji wanachama, Semina n.k. zinafanyika na sasa tupo kwenye majadiliano ya kufunga mkataba wa Kutambuana tukiwa na lengo la kufunga Mkataba wa Hali Bora.

Mshikamano kati ya chama na mwajiri pia nao umekuwa mzuri na mfano mzuri ni kwamba kwenye Mei Mosi ya mwaka huu 2018, kwa mara ya kwanza Mwajiri alichangia TShs.5,000,000/= ili kuiwezesha TUICO kuandaa Mei Mosi Kitaifa Mkoani Iringa.

Chama kwa sasa bado kinaendelea kufuatilia madai ya wafanyakazi hao dhidi ya Serikali ambayo inadaiwa jumla ya fedha za Kitanzania Shilingi Bilioni kumi na saba ambapo mpaka sasa bado tunafanya mazungumzo na Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya madai hayo.

## HITIMISHO

Hatuna budi kukipongeza chama kwa kufanikisha kutatua mgogoro huu dhidi ya Mwekezaji huyo ambao ulidumu takribani miaka kumi na mbili (12) Mahakamni na pia chama kuweza kurudisha mahusiano mazuri na MPM.

Chama kiendeleo na juhudi za kupigania maslahi ya wanachama na wafanyakazi pote nchini.





*Mfanyakazi akisaini Mkataba wake wa ajira*

## JEURI YA TUICO NGUVU YA UMOJA

**Na: Willy Kibona**  
**TUICO DSM**  
**“WAKI wa Utaratibu”**

Nderemo tele TUICO, nyumbani kwake kichama,  
Malezi mema TUICO, wito wangu wanachama,  
Maadili safi TUICO, lengo lake kujituma,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Hongera kwa viongozi, wa TUICO ngazi zote,  
Uoga uepukeni, ndiyo ngao iliyopo,  
Katiba itumieni, na kanuni zilizopo,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Chama kihudumieni, popote pale mlipo,  
Uongo uepukeni, ndiyo ngao iliyopo,  
Katiba itumieni, na kanuni zilizopo,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Naona mwanong’ona, jina langu mwalipanga,  
Mimi Kibona kwa jina, Baba yangu alipanga,  
Nyote karibuni sana, mikakati kuipanga,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Majungu na majigambo, mwiko tusikaribishe,  
Mshikamano ni fimbo, maadui tuwapishe,  
Upendo bila mafumbo, kuziepuka kasheshe,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Eh Mungu nipe uweza, kwa haya niliyonena,  
TUICO si miujiza, bali ni kazi twaona,  
TUICO yajitangaza, kwa utendaji mwanana,  
Hongera chama TUICO. uchaguzi wa kanuni,

TUICO tutende mema, Mungu tupe ujasiri,  
Kazi pasipo unyama, wafanyakazi mwajiri,  
Nidhamu ni kitu chema, wanachama siyo siri,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

Tamati nisiwachoshe, wasomaji jaridani  
Wala sitaki nikeshe, kuwatia mtihani,  
Wanachama mishamishe, TUICO chama makini,  
Hongera chama TUICO, uchaguzi wa kanuni.

... kwa huduma za

- Utetezi
- Elimu
- Kufunga Mikataba

jiunge sasa na **TUICO**



Ilala Sharifu Shamba, S.L.P. 5680, Dar es Salaam.  
Simu: +255 22 2866910, 2866959/60, Fax: +255 22 2866911  
E mail: [tuico2004@yahoo.com](mailto:tuico2004@yahoo.com)

**“Jenga Chama imara na imarisha mshikamano”**